*Wekeza na jenga maisha na SACCOS*

# LESA SACCOS LTD

## REG. No DSR 1299

# SERA YA UWEKEZAJI

WEKA AKIBA MARA KWA MARA, KOPA KWA BUSARA LIPA KWA WAKATI, WEKEZA KWA MAENDELEO YAKO.

TOLEO LA I: 2020

## UIDHINISHAJI WA SERA YA UWEKEZAJI

| Tarehe ya Kupitishwa na Kikao Cha Bodi | | Kikao Cha Bodi cha Tarehe 17 Julai 2020 |
|---|---|---|
| Mpya<br><br>Imehuishwa | ☐<br><br>☐ | Toleo la: I<br>Mwaka 2020 |

**Imetiwa Saini kwa Niaba ya Wanachama na;**

| S/N | Jina | Wadhifa | Tarehe | Sahihi |
|---|---|---|---|---|
| 1 | EVA.J.BOSCO | Mwenyekiti wa Bodi | 23/11/2020 | |
| 2 | GWAMAKA JAPHARI | M/Mwenyekiti wa Bodi | 23/11/2020 | |
| 3 | SEMALY KISAMO | Mjumbe wa Bodi | 23/11/2020 | |
| 4 | SHAFII MMILE | Mjumbe wa Bodi | 23/11/2020 | |
| 5 | NAOMI SERBANTEZ | Mjumbe wa Bodi | | |

**Imetiwa Saini kwa Niaba ya Watendaji na:**

| Jina | Wadhifa | Tarehe | Sahihi |
|---|---|---|---|
| DEONATUS KIHEKA | Meneja | 28/09/2020 | |

**Kwa Matumizi ya Mrajis:**

Maoni ya Mrajis:

| Jina | Wadhifa | Tarehe | Sahihi |
|---|---|---|---|
| | | | |

*Muhuri*

## YALIYOMO

*DIBAJI* ........ iii
SEHEMU YA KWANZA ........ iv
1.0 UTANGULIZI ........ iv
1.1 Historia fupi ya Chama ........ iv
1.2 Wigo na Madhumuni ya Sera ........ iv
1.2.1 Madhumuni ya Sera ya uwekezaji ........ iv
SEHEMU YA PILI ........ v
2.0 MAENEO AMBAYO CHAMA KINATAKIWA KUWEKEZA ........ v
2.1 Maeneo ambayo chama kinaweza kuwekeza ........ v
2.2 Mambo ya kuzingatia kabla ya uwekezaji ........ vi
2.3 Muda wa kuiva wa uwekezaji ........ vi
SEHEMU TATU ........ vii
3.0 HATARI ZINAZOWEZA KUJITOKEZA WAKATI WA UWEKEZAJI ........ vii
SEHEMU YA NNE ........ viii
4.0 MAMLAKA YA KUFANYA UWEKEZAJI NA MGAWANYO WA MAJUKUMU ........ viii
4.1 Mamlaka ya Uwekezaji ........ viii
4.1.2 Mkutano Mkuu wa mwaka wa Chama ........ viii
4.1.3. Bodi ya chama ........ viii
4.2 Mgawanyo wa Majukumu ........ viii
4.2.1 Majukumu ya Bodi ya Chama ........ viii
4.2.2 Majukumu ya Menejimenti ........ viii
SEHEMU YA TANO ........ 7
5.0 UPEMBUZI WA UWEKEZAJI ........ 7
5.1 Kamati ya Muda ya Uwekezaji ........ 7
5.1 Andiko la Mradi ........ 7
SEHEMU YA SITA ........ x
6.0 UTOAJI WA TAARIFA ZA UWEKEZAJI ........ x
HITIMISHO ........ xi

# SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Historia fupi ya Chama

LESA SACCOS LTD ilianzishwa kwa kuzingatia Sheria ya Vyama Vya ushirika Na.20 ya mwaka 2003.Kwa malengo ya kupokea akiba na kutoa Mikopo yenye masharti nafuu kwa wamanachama wake. Mkutano mkuu wa wanachama ndicho chombo cha juu chenye mamlaka katika shughuli zote za chama na kwa kuzingatia Sheria ya Vyama Vya ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 kinatambua kuwa bodi ya chama ndio chombo pekee cha kuongoza chama kwa kuzingatia ukasimishwaji wa madaraka hayo kupitia mkutano mkuu wa wanachama.

Kifungu Na.52 cha Sheria ya Vyama Vya Ushirika kinaenda mbali zaidi na kutoa nafasi kwa bodi kuandaa miongozo mbalimbali ya kusimamia chama na miongoni mwa miongozo iliyotajwa ni pamoja na sera ya uwekezaji.

### 1.2 Mawanda ya Sera

Sera hii inatoa mwongozo wa kisheria na uwazi katika uwekezaji wa aina mbalimbali utakaofanywa na LESA SACCOS LTD kwa kuzingatia Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013, Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Na. 10 ya mwaka 2018 na Kanuni ya Huduma Ndogo za Fedha (SACCOS) ya mwaka 2019.

Sera hii itatumika wakati wote kama mwongozo wa kuzingatiwa wakati wa kufanya maamuzi ya uwekezaji (Investment decisions) kwa maslahi mapana ya wanachama na chama.

### 1.3 Madhumuni ya Sera ya uwekezaji

i. Madhumuni ya sera hii ni kukidhi matakwa ya Sheria na Kanuni lakini pia ni mwongozo wa namna bora kwa Bodi na Menejimenti wanaweza kufanya uwekezaji kwa tija na ufanisi.

ii. Kusaidia bodi ya LESA SACCOS LTD Kuainisha majukumu ya pande zote zitakazohusika katika Uwekezaji.

iii. Kuisaidia bodi ya LESA SACCOS LTD Kuweka utaratibu utakaozingatiwa katika mchakato wa maamuzi ya uwekezaji.

iv. Kusaidia Kuweka uelewa wa pamoja kwa wahusika wote juu ya malengo ya uwekezaji.
v. Kusaidia Kutoa mwongozo na ukomo wa uwekezaji utakaofanywa na LESA SACCOS LTD
vi. Kusaidia Kuweka mwongozo wa kufanya tathimini ya uwekezaji.
vii. Kusaidia Kupima kama uwekezaji uliofanyika unasimamiwa kwa kuzingatia Sheria na Kanuni.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MAENEO AMBAYO CHAMA KINATAKIWA KUWEKEZA

Shughuli kuu ya LESA SACCOS LTD ni kupokea akiba za wanachama na kutoa mikopo kwa wanachama wake. Hivyo kipaumbele cha uwekezaji wa fedha za LESA SACCOS LTD utakuwa ni kutoa mikopo kwa wanachama wake.

### 2.1 Maeneo ambayo chama kinaweza kuwekeza

Chama kitawekeza kwenye maeneo mengine endapo chama kitakuwa na ukwasi toshelevu, hivyo chama kinaweza kuwekeza katika maeneo yafuatayo:

i. Kuwekeza fedha katika benki kama Amana za muda maalumu (FDR).
ii. Kuwekeza kwenye taasisi nyingine za kifedha kama vile ununuzi wa vipande UTT au hisa katika kampuni zinazofanya vizuri katika soko la Hisa (DSE).
iii. Kuwekeza katika dhamana za Serikali (Government Securities).
iv. Kuwekeza kwenye SACCOS zilizopata leseni daraja "B" na Vyama vya Ushirika vya upili (second tier or secondary cooperative societies)
v. Kuwekeza katika hisa za Vyama vingine vya Ushirika hususani Vyama vya Upili (Unions) na Shirikisho (Federations)
vi. Kuwekeza katika Hati Fungani za Serikali (Treasury Bills & Bonds)

vii. Kuwekeza katika Hati Fungani za Kampuni za Umma (Corporate Bonds)

viii. Kuwekeza katika mali zisizozalisha (Non-Earning assets) kama vifaa, majengo na ardhi ambapo;

a) Chama kitawekeza katika mali zisizozalisha (non-earning assets/property/Equipment) kwa kiwango kisichozidi asilimia 10 % ya mali zote za chama.

b) Uwekezaji katika ardhi na majengo hautazidi asilimia 5% ya mali zote za chama.

Aidha, LESA SACCOS LTD inaweza kuwekeza katika mradi wowote ambao utaruhusiwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika.

## 2.2 Mambo ya kuzingatia kabla ya uwekezaji

Kabla ya kufanya maamuzi ya kuwekeza, chama kitafanya upembuzi wa kina kikizingatia mahitaji na hali halisi ya ukwasi na vipindi vya mahitaji makubwa ya mikopo kwa wanachama. Chama kitakapohitaji kuwekeza, kitapaswa kuzingatia mambo yafuatayo:-

i. Kufanya tathimini ya kina juu ya mahitaji na uwezo wa kifedha wa chama.

ii. Muda wa kuiva kwa uwekezaji (Investment Maturity).

iii. Mapato tarajiwa toka kwenye uwekezaji husika (Return on investment).

iv. Vihatarishi kwenye uwekezaji (Investment risks).

v. Utendaji wa taasisi/kampuni husika (Performance trend analysis).

vi. Sera za uwekezaji za Sekta husika.

vii. Historia ya Taasisi husika.

viii. Gharama za uwekezaji.

ix. Na mambo mengine kulingana na mazingira husika.

## 2.3 Muda wa kuiva kwa uwekezaji

LESA SACCOS LTD itafanya uwekezaji usiozidi miezi 12 na kila mwisho wa kipindi tathmini ya hali ya ukwasi wa Chama itafanywa ili kubaini mahitaji, ulazima na fursa ya kuhuisha uwekezaji husika. Uhuishaji wa uwekezaji unaweza kufanywa kwenye Taasisi nyingine inayotoa riba/faida kubwa

zaidi kwa wakati husika mara baada ya kufanya upembezu. LESA SACCOS LTD itaweza kuwekeza katika maeneo mengine ambayo muda wa uwekezaji utazingatia miongozo itakayotolewa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika.

### 2.4 Ukomo wa Uwekezaji

i. Uwekezaji wa LESA SACCOS LTD katika Vyanzo vinavyozalisha riba hautazidi uwiano wa 30% ya Jumla ya Mali za Chama kwa mujibu wa Sera hii na ili kuwezesha fedha nyingi zitolewe kama mikopo kwa Wanachama

ii. Uwekezaji wa LESA SACCOS LTD katika mali zisizozalisha (non-earning assets) hautazidi uwiano wa 10% ya Jumla ya Mali za Chama

iii. Uwekezaji wa LESA SACCOS LTD katika ardhi na majengo hautazidi uwiano wa 5% ya Jumla ya Mali za Chama.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 NAMNA YA KUPUNGUZA VIHATARISHI

LESA SACCOS LTD inafanya uwekezaji kwenye maeneo tofauti tofauti (Portfolio diversification) ili kupunguza hatari ya kupata hasara kubwa. Hivyo, uwekezaji huu unazingatia mambo matatu ambayo ni usalama, ukwasi na faida tarajiwa. Usalama wa uwekezaji umekuwa ndio lengo kuu la mpango wa uwekezaji.

Ili kupunguza hatari katika uwekezaji LESA SACCOS LTD imezingatia mambo yafuatayo:-

i. LESA SACCOS haijaweka fedha katika benki moja au taasisi moja ya kifedha kwa kiwango kinachozidi asilimia 25% ya mtaji tete wa chama kwa ajili ya kufanya mtawanyo wa vihatarishi (diversification of risks or risks spread).

ii. LESA SACCOS LTD inawekeza kwenye maeneo salama yaliyotajwa kwenye Sera hii katika sehemu ya pili.

iii. LESA SACCOS LTD inatarajia kufanya uwekezaji kwenye dhamana za muda mfupi na mrefu, masoko ya fedha (money market) na kudhibiti muda wa uwekezaji.

## SEHEMU YA NNE

# 4.0 MAMLAKA YA KUFANYA UWEKEZAJI NA MGAWANYO WA MAJUKUMU

## 4.1 Mamlaka ya Uwekezaji

### 4.1.2 Mkutano Mkuu wa mwaka wa Chama

Mkutano Mkuu wa mwaka wa LESA SACCOS LTD ndiyo wenye mamlaka ya kupitisha aina yoyote ya uwekezaji unaotakiwa kufanywa na Chama. Aidha, baada ya Mkutano Mkuu kupitisha, Chama kitatakiwa kupeleka maombi ya kuidhinishiwa uwekezaji huo kwa Mrajis.

### 4.1.3. Bodi ya chama

Bodi ya LESA SACCOS LTD itakasimishwa kufanya uwekezaji kwa niaba ya Wanachama. Hivyo, Bodi itapaswa kuzingatia maazimio na maelekezo ya Mkutano Mkuu wa chama.

## 4.2 Mgawanyo wa Majukumu

### 4.2.1 Majukumu ya Bodi ya Chama

Bodi ya LESA SACCOS LTD itakuwa na jukumu la kuelekeza na kusimamia uwekezaji wa Chama. Bodi itatekeleza majukumu yake kwa maslahi ya Chama kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Masharti ya Chama. Majukumu ya Bodi kwenye utekelezaji wa Sera hii yatakuwa kama ifuatavyo:

i. Kufanya tathimini ya vihatarishi katika uwekezaji na mipaka ya uwekezaji na kutoa taarifa kwa pande zote zinazohusika.
ii. Kuisimamia Menejimenti ya Chama katika uendeshaji wa mradi.
iii. Kuandaa taarifa ya maendeleo ya uwekezaji na kuiwasilisha kwenye Mkutano Mkuu wa wanachama.
iv. Kujadili hali ya mwenendo wa uwekezaji kwenye vikao vya Bodi vya kila robo mwaka.
v. Kushauri wanachama juu ya fursa nyingine za uwekezaji.

### 4.2.2 Majukumu ya Menejimenti

Menejimenti ya LESA SACCOS LTD itawajibika kwa Bodi ya Chama na itakuwa na majukumu yafuatayo:

i. Kutekeleza maamuzi ya uwekezaji yaliyofikiwa na Bodi.

ii. Utunzaji wa kumbukumbu na uandaaji wa taarifa za fedha za uwekezaji na kuziwasilisha kwa Bodi.
iii. Kupendekeza kwa Bodi fursa zozote za uwekezaji kulingana na mwenendo wa uchumi uliopo.
iv. Kufuatilia na kutoa taarifa kwa Bodi juu ya maendeleo na shughuli za uwekezaji mara kwa mara.
v. Kushauri Bodi kufanya mapitio na maboresho ya Sera hii.
vi. Kuwasilisha taarifa kwa Bodi juu ya mabadiliko makubwa ambayo yanaweza kuathiri ufikiaji wa malengo ya uwekezaji wa chama.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 UPEMBUZI WA UWEKEZAJI

### 5.1 Kamati ya Muda ya Uwekezaji

Kabla ya kufanya maamuzi ya kuwekeza, Bodi ya Chama itafanya upembuzi wa kina na itazingatia mahitaji na hali halisi ya ukwasi na vipindi vya mahitaji makubwa ya mikopo kwa wanachama kama sera ya Menejimenti ya Ukwasi,Mali na Dhima inavyoelekeza. Aidha, ili Bodi ifanye uwekezaji kwa ufanisi ni muhimu kuunda Kamati ndogo ya muda kwa ajili ya kufanya ufuatiliaji wa mambo mbalimbali yanayohusiana na uwekezaji. Kamati hii itakuwa na Wajumbe watatu (3) wanaoundwa kutokana na Wajumbe 2 wa Bodi pamoja na Meneja.

### 5.2 Andiko la Mradi

Sera hii ni mwongozo wa jumla haiwezi kuelezea masuala ya kitalaam kwa kila aina ya uwekezaji. Kwa maana hii, kila aina ya uwekezaji LAZIMA iwe na andiko la mradi ili kufanya upembuzi yakinifu wa faida na hasara za uwekezaji husika lakini pia uwezo wa Chama kuwekeza na uzingatiaji mahitaji ya Sheria na Kanuni. Andiko la Uwekezaji linavipengele vifuatavyo;-

(i) Aina ya uwekezaji
(ii) Muda wa kuiva
(iii) Eneo la uwekezaji (proximity)

(iv) Kiwango cha riba
(v) Mtaji unaohitajika
(vi) Vyanzo vya mtaji huo wa kuwekeza bila kuathiri utoaji wa huduma za mikopo kwa Wanachama
(vii) Upembuzi wa vihatarishi vya kiuchumi na kisiasa katika uwekezaji
(viii) Umiliki wa uwekezaji
(ix) Ainisho la gharama zitakazotumika katika mchakato wa kuwekeza hadi kufikia hatua ya kupata faida
(x) Faida inayotarajiwa (faida za kifedha na zisizo za kifedha)
(xi) Upembuzi yakinifu wa faida na hasara
(xii) Namna tathmini ya uwekezaji itakavyokuwa inafanyika
(xiii) Uidhnishwani wa andiko la mradi wa uwekezaji (Bodi)

## SEHEMU YA SITA

## 6.0 UTOAJI WA TAARIFA ZA UWEKEZAJI

Menejimenti ya LESA SACCOS LTD itatakiwa kutoa taarifa ya uwekezaji kwa Bodi ya chama angalau kila mwezi au isizidi robo mwaka. Taarifa hiyo itaainisha mambo yafuatayo;

i. Aina zote za uwekezaji uliofanywa na chama.
ii. Riba halisi ya kila uwekezaji mpaka siku taarifa hiyo inapotolewa.
iii. Tarehe ya kuiva kwa kila uwekezaji na taarifa nyingine zinazohusiana na uwekezaji.
iv. Shughuli za uwekezaji za kila mwezi kama vile kununua na kuuza, na riba iliyorejeshwa.
v. Malinganisho ya kwenye vitabu (book value) na malinganisho ya soko kwa wakati husika (current market value).
vi. Na taarifa nyingine muhimu kama zipo.

## SEHEMU YA SABA

### 7.0 Uidhinishwaji wa Sera

Sera hii imetayarishwa na kupitishwa na Bodi ya LESA SACCOS LTD kwa niaba ya wanachama kwa kibali cha Mrajis MA.82/309/163/06 katika kikao chake kilichofanyika tarehe 17 Julai 2020 na itaanza kutumika baada ya kuidhinishwa na kusajiliwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika.

……………………… **Mwenyekiti**

……………………… **Meneja**

LESA SAVINGS & CREDIT COOPERATIVE SOCIETY LTD
23 NOV 2020
KINONDONI
DAR-ES-SALAAM

……………………………………

**Mrajis wa Vyama vya Ushirika**

Tarehe………………………

TANZANIA
Approved this 20TH
day of JANUARY 2021
Asst. Registrar of Cooperative Societies